SHULE YA SEKONDARI KATE,
S.L.P 194,
NAMANYERE.
TAREHE:14/12/2021.
Simu: 0765058784/ 0623978145/0628146221.

Kumb. Na. *KSS/US/KDT-I/2018/VOL.1/01*
Jina la mwanafunzi.....
S.L.P 6,
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KATE, WILAYA YA NKASI, MKOA WA RUKWA MWAKA 2021.

1.0 Utangulizi

Ndugu.....nafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Kate kidato cha kwanza, mwaka 2021. Shule itafunguliwa tarehe 11 – 01 – 2021 na mwisho wa kuripoti nitarehe /01/2021.

2.0 Mambo muhimu yakuzingatia

2.1 **SARE ZA SHULE**

A) Wavulana

i. Suruali mbili(2), moja ya kijanijeshi na moja nyeusi pamoja na mashati mawili(2) meupe tetroni mikono mifupi.
ii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visiginovifupi na vinene pamoja na soksi nyeupe pea mbili (2).
iii. Sweta la bluu lenye shingo ya**'V'**

B) Wasichana

i. Sketi mbili (2), moja ya kijanijeshi na moja nyeusi(kitambaa kizito) pamoja na mashati mawili meupe tetroni mikono mifupi.
ii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vinene pamoja na soksi nyeupe pea mbili (2).
iii. Nguo za kufanyia kazi(shamba dress), Gauni(satini) rangi ya kijani na damu ya mzee
iv. Sweta la bluu lenye shingo ya**'V'**
v. **Kwa Hostel mwanafunzi aje na ndoo mbili ndogo na vyombo vya chakula.**

C) SARE ZA MICHEZO

Wavulana kwa wasichana wanatakiwa kuwa na truck-suit za bluu na raba kwa ajili ya michezo(zitatumika kwasiku za michezo)

2.2 VIFAA VYA DARASANI (TAALUMA)

Daftari kubwa zisizopungua kumi, kalamu za wino za bluu au nyeusi, kalamu ya risasi pamoja na mkebe (Mathematical set).

2.3 MAHITAJI YA CHAKULA .

Pamoja na serikali kugharamia michango yote ya mwanafunzi shuleni, mzazi/mlezi utawajibika kugharamia michango ya **chakula** ili mwanao aweze kupata **uji na chakula cha mchana** shuleni(kwakuwa mwanao hatakaa hosteli utapaswa kulipa nusu ya michango hiyo kwa kila kifungu). Kwa ujumla michango ya chakula kwa mwaka ni kama ifuatayo

i.Mchango wa pesa ya upishi Tsh.54,000/=(Hamsini na nne elfu tu) kwa mwaka,Tsh.27000/= kwa muhula na Tsh.13500/= kwa robo muhula na siyo chini ya hapo.

ii.Mahindi sado 50 kwa mwaka au sado 25 kwa muhula au sado 12 ½ kwa robo mwaka na sichini ya hapo.

iii.Maharage sado 15 kwa mwaka au sado 7 ½ kwa muhula au sado zisizopungua 4 kwa robo mwaka.

NB:

- ***Tafadhali, michango hiyo inatakiwa iwasilishwe kwa wakati kwa kamati ya chakula ya wazazi.Pia kukaa hosteli sio lazima ni hiari.***
- ***KWAMWAKA HUU 2021 HAKUTAKUWA NA NAFASI YA HOSTELI KWA WANAFUNZI WOTE WANAOKUJAKUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA, WANAFUNZI WOTE WATATAKIWA KUTOKEA NYUMBANI.***

- **UNATAKIWA KUHAKIKISHA UTAKAPOKUJA KURIPOTI NA MWANAONILAZIMA UJE NA MCHE WA MATUNDA AINA YOYOTE (MIPARACHICHI NI MUHIMU ZAIDI).**
- **HAKIKISHA UNAKUJA NA CHETI CHA KUZALIWA CHA MWANAO SIKU YA KURIPOTI SHULENI.**
- **MUDA WA KUMLETA MWANAFUNZI SHULENI NI KUANZIA JUMA TATU HADI IJUMAA KWAMASAA YA KAZI KUANZIA SAA 2.00 ASUBUHI HADI SAA 9.30 JIONI.ZINGATIA MUDA HUO.**

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

A: UTANGULIZI

Sheria za shule zinazingatia sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995 (3).

B: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Sheria na kanuni za shule zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII na TABIA NJEMA kwa ujumla. Hivyo basi wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia, kauli na vitendo. Nazo ni kama ifuatavyo;

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama anapomsalimu Mwalimu, Mtumishi wa shule au mtumishi yeyote aliyemzidi umri.
2. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi;
    a) Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya
    b) Kufuga kucha na nywele ndefu na chafu.
    c) Kufuga ndevu
    d) Kunyoa kipara
    e) Kunyoa kiduku
    f) Kumpiga mwenzake
    g) Kutukana
    h) Kutia dawa nywele (Curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
    i) Kuvaa kofia shuleni, kuvaa mapambo/urembo (mfano; Heleni, Bangili, nk) akiwa shuleni.
    j) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu.
    k) Kuvaa kaptura na kandambili akiwa darasani au katika ofisi zote za shule.
    l) Kuvaa suruali chini ya kiuno.
    m) Kuvaa nguo za mitindo, Mfano; MODEL
4. Mwanafunzi atasimama mstarini wakati wa kupata huduma kama chakula.
5. Mwanafunzi anatakiwa kunyoosha mkono juu na kusimama kila anapouliza au kujibu swali darasani.
6. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtulivu, asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyosababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa: Darasani, Maktaba, Bwenini, Wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano ; PAREDI nk.
7. Mwanafunzi LAZIMA awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Hivyo mwanafunzi:
   Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya;
    a) Kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
    b) Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa.

h) Kufanya kosa lolote lililo kinyume na maadili bila kujali kama aliwahi kutumikia kosa hilo au hapana.
i) Kuanzisha, kuchochea au kushiriki migomo au fujo shuleni, kuvuruga amani na utulivu wa watu/shule.
j) KUWA NA SIMU YA MKONONI AU KUKUTWA NA VIAMBATISHI VYAKE (kama charger, betri, vocha, line, ear phone, n.k)
k) Kukataa adhabu halali itolewayo na mwalimu.
l) Kutoroka na kulala nje ya shule kwa wanafunzi wa Hostel.
m) Kutohudhuria shule kwa muda mrefu.
n) Kupiga, kupigana na mwalimu au mfanyakazi wa shule au mwanafunzi mwenzake au mtu yeyote.

NB: makosa yanatokana na kanuni ya elimu ya mwaka 2014 inayotoa mwongozo kuhusu mambo ambayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule

KARIBU SANA SEKONDARI YA KATE
"KATIKA ELIMU, USHINDI NI LAZIMA"

.....
MWENDA, G
MKUU WA SHULE.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KATE
NKASI

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
SHULE YA SEKONDARI KATE

FOMU YA KUKIRI UTII

Mimi..... ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Kate, *nipo/sipo tayari kutii sheria na kanuni zote za shule kama zilivyooneshwa.

Sahihi ..... Tarehe.....

Mimi ..... mzazi/mleziwa .....
*Nipo/sipo tayari kumpa huduma/mahitaji yote aweze kuendelea na masomo yake, shule ya Sekondari Kate .

Sahihi ..... Tarehe.....

Futa isiyohusika

"USIJE BILA KUKAMILISHA FOMU HII"

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TO THE MEDICAL OFFICER,
……HOSPITAL,
BOX……
……..

Please examine the student……
The following:-

a) Epilepsy……
b) Vision ……...
c) Hearing ……
d) Pregnancy ……
e) Any other problem that can lead him / her not to be able for schooling/any other health problem that will require him/her to stay close to hospital.

DOCTOR'S DECLARATION.

I have examined the above mentioned student. He /she is fit/not fit for schooling.

Signature …….. Title……
Date ……..